

## OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, MANISPAA YA MOROGORO

### UTARATIBU WA UFUGAJI WA SAMAKI

**Kwa Kuzingatia Kanuni za Uvuvi za Mwaka 2009, Sehemu ya Nne: Maendeleo na Usimamizi wa Ufugaji wa Samaki.**

#### MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KABLA HUJAANZA UFUGAJI WA SAMAKI

Mara unapoamua kufuga samaki, unahitaji maarifa, kabla hujaanza kujenga bwawa ni vizuri ukatafuta msaada kutoka ofisi ya uvuvi wa samaki au mfugaji samaki mwenye uzoefu. Ushauri wao unaweza kukusaidia uwe mfugaji wa samaki mwenye kufanikiwa. Mambo muhimu ya kuangalia unapotaka kufuga samaki ni kama yafuatayo;

**Maji;** Ni muhimu eneo linalochaguliwa liwe na maji ya kutosha nayakuaminika ili pale yanapohitajika yanapatikana kwa wakati. Ni lazima maji yawepo kwa mwaka mzima kwa ajili ya samaki. Vyanzo vizuri kwa ajili ya bwawa la samaki ni chemchemi, mito na maji ya ardhini.

**Udongo;** Udongo wa mfinyanzi ni mzuri sana kwa mabwawa kwa sababu unahifadhi maji kwa muda mrefu, udongo wa mchanga mtupu haufai kwasababu unaruhusu maji kunywea kirahisi.

**Eneo;** Eneo lisiwe na historia ya mafuriko, mafuriko yakitokea samaki wanaokuwa bwawani wataondoka na maji na bwawa litafunikwa na udongo. Unaweza ulizia kwa watu wa eneo husika ili kupata historia yake.

**Hali ya hewa;** Joto la maji ya bwawa ni muhimu sana katika ukuaji wa samaki. Samaki aina ya Tilapia hukua vizuri katika maji yenye uvuguvugu (kati ya nyuzi joto 25-30).

**Usalama;** Ni vizuri eneo liwe karibu na nyumbani ili kudhibiti wezi na maadui wa samaki, hili pia huwezesha kutoa huduma kwa urahisi. Pia eneo linatakiwa kuwa ni la amani na ambalo kunakuwa na maelewano baina yake na wakazi wengine kinyume na hapo, iwapo hakutakuwepo na maelewano maadui zako wanaweza kuwadhuru samaki unaowafuga.

**Upatikanaji wa vifaranga vya samaki;** Umakini mkubwa unahitajika ili kupata vifaranga vya samaki ambavyo vitaweza kuwa na uwezo wa kutoa angalau gramu 500 au zaidi baada ya miezi sita mpaka nane ya ukuaji. Wapo wazalishaji wengi wa mbegu za vifaranga kwa mfano Tanzania Fisheries Research Institute (TAFIRI) (Nyegezi, Mwanza), Kingolwira na Ruvu hivi ni baadhi tu ya vituo vya uzalishaji wa vifaranga vya samaki.

#### FAIDA ZA UFUGAJI WA SAMAKI

1. Kuongeza ajira na kipato
2. Husaidia katika kuimarisha lishe kwa binadamu na mifugo mbalimbali (mfano hutumika kwenye chakula cha kuku, nk)

#### SHERIA

1. Kuna ulazima wa kuzingatia sheria zote za mazingira ili kutoathiri mazingira na maeneo jirani.
2. Mhusika anatakiwa awe na leseni ya biashara ya Manispaa, anayoipata kutoka ofisi ya biashara ya Manispaa ya Morogoro.
3. Mhusika anatakiwa awe na leseni ya kujishughulisha na uuzaji wa samaki, anayoipata kutoka ofisi ya mifugo na uvuvi iliyopo Manispa ya Morogoro kwa shilingi 20,000 kwa mujibu wa Sheria ya Mwaka 2003 na Kanuni za Uvuvi za Mwaka 2009
4. Hati ya kusafirisha samaki na mazao yake hailipiwi.



#### UTARATIBU WA KUJISHUGHULISHA NA BIASHARA YA SAMAKI NA MAZAO YAKE

1. Kuwe na vigae kwenye sakafu na ukutani
2. Kuwe na msumeno wa kukatia samaki
3. Kuwe na mzani wa kidigitali
4. Kuwe na jokofu la kuhifadhi samaki
5. Kuwe na ndoo inayotiririsha maji
6. Mfanyabiashara huyo awe na sare
7. Awe na cheti cha afya

#### TARATIBU ZA KUSIMAMIA UTEKELEZAJI

Faini ya kufanya biashara ya samaki na mazao yake bila leseni ni kati ya Tshs. 200,000 na Tshs.1,000,000